

# K.C.S.E 2007 KISWAHILI KARATASI YA 102/3

1. **(Lazima)**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:**

- 1 Tohara, usimwazie, mwanamke,  
Tohara, usikaribie, mwili wake,  
Tohara, usiifikie, ngozi yake,  
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!
- 2 Tohara, hiyo haramu, adha kwake,  
Tohara, ni kubwa sumu, si kufu yake,  
Tohara, ni za kudumu, dhara zake,  
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!
- 3 Tohara, kile kijembe, usikishike,  
Tohara, yule kiumbe, si haki yake,  
Tohara, usintimbe, kwayo makeke,  
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!
- 4 Tohara, ni tamaduni, usiyashike,  
Tohara, ati uzimani, ajumuike,  
Tohara, umaaluni, kwa mwanamke,  
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!
- 5 Tohara, akijifungua, ataabike,  
Tohara, yaweza ua, hufa wanawake,  
Tohara, inausumbua, uhai wake,  
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!
- 6 Tohara, na siku hizi, haya uyashike,  
Tohara, gongjwa umaizi, lije limshike,  
Tohara, ageuke uzi, huo mwili wake,  
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!
- 7 Tohara, nasisitiza, mwanamke,  
Tohara, inaibeza, hadhi yake,  
Tohara, inadumaza, fikira yake,  
Tohara ya mwanamke, zamu yake ipitile!

- (a) Eleza dhamira ya msanii katika shairi hili. (alama 2)
- (b) Fafanua madhara manne ya tohara kwa mwanamke. (alama 4)
- (c) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi. (alama 4)
- (d) Kulingana na mshairi, mwanamke hupashwa tohara kwa nini? (alama 2)
- (e) Andika ubeti wa ska katika lugha nathari. (alama 4)
- (f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi

- (i) adha  
(ii) Usimtimbe (alama 2)

(g) Upashaji wa tohara kwa mwanamke ni mojawapo ya maswala ibuka katika jamii yetu. Taja maswala ibuka mengine mawili yanayohusu mwanamke. (alama 2)

### RIWAYA

#### BURHANI: Mwisho wa Kosa

#### Jibu swali la 2 au la 3

2. Onyesha jinsi ukengeushi unavyojitokeza katika riwaya ya Mwisho wa Kosa. (alama 20)
3. Eleza jinsi ambavyo KINAYA kimetumiwa katika riwaya ya Mwisho wa Kosa. (alama 20)

### TAMTHILIA

#### KITHAKA WAMBERIA: Kifo Kisimani

#### Jibu swali la 4 au la 5.

4. Ukirejelea tamthilia ya Kifo Kisimani, fafania mambo yanayopiganiwa na umma katika nchi ya Butangi. (alama 20)
5. "Uovu wa mume si uovu wa mke"
- (a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)
- (b) Onyesha jinsi mhusika anayerejelewa hapa alivyosaidia kupunguza mateso ya wana Butangi. (alama 10)
- (c) Eleza wasifu wa msemaji. (alama 6)

### HADITHI FUPI

#### K.W. WAMITILA: Mayai Waziri wa Maradhi

6. "Mimi nashughulika na wanyama wa porini, mambo yanayohusu binadamu mimi simo".
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- (b) Onyesha jinsi mzungumzaji na wenzake wasivyowajali wananchi wanaowahudumia. (alama 16)

### FASIHI SIMULIZI

7. (a) Nini maana ya mighani/migani? (alama 4)
- (b) Fafania sifa tano za mighani/migani. (alama 10)
- (c) Eleza umuhimu wa mighani/migani. (alama 6)